# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 28 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Juni 2025

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


## ZAIDI YA TANI 1,900.000 MBOLEA YA RUZUKU ZATOLEWA MIAKA MITATU



Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2025/26 ya shilingi trilioni 1.24 Mei 21, 2025 Bungeni jijini Dodoma.


NDANI>>

Tanzania kuwa kitovu cha mbolea ifikapo 2030 4

Wazalishaji wa Mbolea waaswa kutunza na kuwasilisha Takwimu za Uzalishaji TFRA 16






# TANI 1,900.000 MBOLEA ZATOLEWA

Katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2024/25, serikali imetoa mbolea ya ruzuku yenye jumla ya tani 1,454,974.721 zenye thamani ya shilingi 708,627,762,436 kwa wakulima wa mazao yote nchini.



Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2025/26 ya shilingi trilioni 1.24 Mei 21, 2025 Bungeni jijini Dodoma.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akiwasilisha makadirio na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2025/26 alieleza Bunge kwamba utekelezaji wa mpango wa ruzuku umechangia ongezeko kubwa la matumizi ya mbolea kutoka tani 363,599 mwaka 2021/2022 hadi tani 848,884 mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia 133.47.

Waziri Bashe aliliomba Bunge liidhinishe shilingi trilioni 1.24 kwa matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2025/26.

Alisema uzalishaji wa ndani wa mbolea umeongezeka kutoka tani 32,230 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 158,628 mwaka 2024/25, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 392.

Alieleza kuwa mafanikio hayo yamechangiwa na kuanzishwa kwa kiwanda cha Itracom kilichopo Nala, jijini Dodoma, pamoja na upanuzi wa kiwanda cha Minjingu, ambacho kimeongeza uwezo wake wa uzalishaji kutoka tani 30,000 hadi 100,000 kwa mwaka.

Kutokana na ongezeko la uzalishaji, Waziri alisema upatikanaji wa mbolea umeimarika kutoka tani 678,017 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 1,213,729 mwaka 2024/25, ambalo ni ongezeko la asilimia 79.

Pia, Waziri Bashe abainisha kuwa matumizi ya mbolea kwa hekta yameongezeka kutoka kilo 19 mwaka 2021/2022 hadi kilo 24 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 26.

Kuhusu urasimishaji wa wakulima wadogo, Waziri alisema serikali ilipanga kurasimisha wakulima 10,000 kwa mwaka wa fedha 2024/25 kwa kuwapatia hati za hakimiliki za ardhi na kubainisha kuwa hadi Aprili, 2025 Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wamepima jumla ya mashamba ya wakulima 9,117 waliokuwa wamepimiwa ardhi na kupatiwa hati za hakimiliki za ardhi katika Halmashauri za Iramba (Singida), Mbinga (Ruvuma), Songwe (Songwe), na Chamwino (Dodoma).

Akizungumzia usajili wa wakulima na wadau wengine wa pembejeo, Waziri alisema hadi sasa wakulima 4,522,011 wamesajiliwa kwenye mfumo wa pembejeo za kilimo. Aidha, waagizaji wa mbolea 64, wasambazaji 7,147 na vyama vya ushirika 720 tayari vimesajiliwa ili kurahisisha usambazaji wa pembejeo kwa wakulima nchini.

# HABARI PICHA WAKATI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO



Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli (kushoto) akifuatilia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (hayupo pichani) alipokuwa akiwasilisha bungeni Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za wizara hiyo kwa Mwaka 2025/2026 tarehe 21 Mei, 2025.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, Dkt. Anthony Diallo, akifuatilia uwasilishwaji wa Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb), kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2025/26 Bungeni Jijini Dodoma Mei 21, 2025.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA, Joel Laurent (katikati) akifuatilia uwasilishwaji wa Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb), kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2025/26 Bungeni Jijini Dodoma Mei 21, 2025.

# HABARI PICHA WAKATI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO





Viongozi mbalimbali walihudhuria wasilisho la Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, yaliyowasilishwa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, Bungeni jijini Dodoma.

# Tanzania kuwa kitovu cha mbolea ifikapo 2030

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Anthony Diallo amesema, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea ya urea unaotarajiwa kutekelezwa na Kampuni ya ESSA ya nchini Indonesia, ni hatua muhimu ya kufikia maono ya nchi kuwa kitovu cha uzalishaji na usambazaji wa mbolea Afrika Mashariki na Kati.

Dkt.Diallo amesema hatua hiyo inakwenda sambamba na kutatua changamoto zinazolikabili soko la mbolea nchini.

Dkt. Diallo ametoa kauli hiyo leo, tarehe 19 Mei 2025, katika hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya awali ya mauziano ya gesi kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya ESSA Industries, iliyofanyika katika hoteli ya Hyatt Regency, jijini Dar es Salaam.

Ameeleza kuwa, kwa muda mrefu Tanzania imekuwa ikitegemea mbolea kutoka nje ya nchi, jambo ambalo limesababisha matumizi makubwa ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza pembejeo hiyo muhimu kwa kilimo.

“Kujengwa kwa kiwanda hiki kutapunguza utegemezi wa mbolea ya uagizaji, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu,” amesema Dkt. Diallo.

Ameongeza kuwa viwanda vingi vya ndani vinategemea mbolea ya urea kama malighafi, hivyo upatikanaji wake wa uhakika kupitia uzalishaji wa ndani utakuwa chachu ya maendeleo ya sekta ya kilimo na viwanda nchini.




Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa TPDC, Derick Moshi (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Essa Rahul Puri wakionesha hati za makubaliano ya awali mara baada ya kuwema sahihi zao kuashiria nia ya TPDC kuiuzia gesi kampuni hiyo kwa ajili ya kutengeneza mbolea ya Urea ifikapo mwaka 2030



Mwenyekiti wa bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Anthony Diallo akizungumza wakati wa hafla ya kusaini makubaliano ya awali ya mauziano ya gesi baina ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), na kampuni ya ESSA Industries iliyofanyika katika ukumbi wa Kilimanjaro Jijini Dar es Salaam tarehe 19 Mei, 2015

Dkt. Diallo amesisitiza kuwa, kwa kutumia rasilimali ya gesi asilia, Tanzania sasa ipo katika nafasi nzuri ya kuzalisha mbolea ya urea kwa wingi, hatua itakayosaidia kuimarisha usambazaji wa mbolea sokoni, kupunguza gharama kwa wakulima na kuleta ustawi wa uchumi wa nchi kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ESSA, Bw. Rahul Puri ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano uliowezesha hatua ya awali ya makubaliano ya mauziano ya gesi, na kueleza kuwa hatua inayofuata ni kufanya utafiti wa kina kuhusu kiasi cha gesi kitakachohitajika kwa uzalishaji wa mbolea.

Amebainisha kuwa, ushirikiano kati ya TFRA, TIC, TFC na TPDC ndio msingi wa mafanikio ya uwekezaji huo unaotarajiwa kugharimu takribani Dola za Marekani bilioni 1.4 na kukamilika ifikapo mwaka 2030.

Naye Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa TPDC, Bw. Derick Moshi amesema shirika hilo litaendelea kuhakikisha upatikanaji wa gesi kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea unakuwa wa uhakika, huku likihakikisha malengo ya uwekezaji huo yanafikiwa.

Kwa upande wake, Bw. Lameck Borega kutoka Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), amesema mradi huo una faida kubwa kwa nchi, ikiwemo kuongeza uhakika wa upatikanaji wa pembejeo hiyo muhimu kwa wakulima kwa wakati tofauti na sasa ambapo upatikanaji wake unakinzana na msimu na mahitaji ya mkulima.

# Habari katika picha, Halfa ya kusaini makubaliano ya mauziano ya gesi baina ya TPDC NA ESSA Industries










# DUMISHENI MSHIKAMANO KWENYE UTENDAJI; MKURUGENZI MTENDAJI TFRA



Watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania wametakiwa kuimarisha mshikamano na ushirikiano baina yao ili kufanikisha malengo ya taasisi hiyo katika kuimarisha tasnia ya mbolea nchini,Huo ni wito uliotolewa na.Mkurugenzi Mtendaji, Joel Laurent, wakati wa kikao kazi cha Mamlaka hiyo kilichofanyika Mei 7, 2025 kwenye Ukumbi wa Maabara jijini Dar es Salaam.

Laurent alisema kwa kiasi kikubwa anaridhishwa na utendaji wa watumishi wa TFRA, jambo lililofanmikishwa kupungua kwa malalamiko kutoka kwa wadau na kuboreshwa kwa huduma kwa wakulima.

Akisisitiza umuhimu wa mshikamano, alirudia kauli mbiu yake isemayo "None of us is as good as all of us", akieleza kuwa kila mtumishi ana mchango muhimu katika kutekeleza majukumu ya Mamlaka kama ilivyokasimiwa kisheria.

Akibainisha mafanikio yaliyopatikana katika msimu wa kilimo 2022/23 na 2023/24, Laurent alisema kuwa kupitia mifumo ya Fertilizer Information System (FIS) na Mfumo wa Kidigitali wa Pembejeo za Kilimo, TFRA imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufuatilia mnyororo mzima wa mbolea kutoka zinapoingia nchini hadi kwa mkulima wa mwisho.

Pia, alieleza kuwa uzalishaji wa mbolea kwa viwanda vya ndani umeongezeka kutoka tani 100,000 mwaka 2022/2023 hadi tani 232,000 mwaka 2023/2024, huku matumizi ya mbolea yakiongezeka kutoka tani 580,000 hadi 840,000 kwa kipindi hicho na mengine mengi.

Aliimwagia sifa Idara ya Huduma za Mamlaka kwa kuandaa mafunzo ya maadili na afya mahali pa kazi ambayo yatasaidia kuimarisha utendaji na kuwawezesha watumishi kuepuka changamoto za kiafya zinazosababishwa na mazingira ya kazini na kifamilia.

Aliwasihi watumishi kutumia changamoto wanazokutana nazo kama fursa ya kujifunza na kuboresha utendaji, huku wakizingatia kasi ya mabadiliko ya teknolojia ili wasiwe nyuma.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mamlaka, Victoria Elangwa aliisifu hotuba nzuri ya Mkurugenzi Mtendaji yenye maelekezo na akaahidi kuyafanyia kazi.

# HABARI KATIKA PICHA WAKATI WA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TFRA NA KIKAO BAINA YA WAFANYAKAZI NA MENEJIMENTI

















# Diallo awashauri wakulima kupima afya ya udongo



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, Dkt. Anthony Diallo, akizungumza na wakulima wa Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Miwa (AMCOS) cha Mkula, Halmashauri ya Ifakara mkoani Morogoro wakati wa ziara iliyolenga kujifunza, kupokea na kutatua changamoto za wakulima hao wa miwa Me 26,, 2025.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Anthony Diallo, amewashauri wakulima wadogo wa miwa kupima afya ya udongo wa mashamba yao kabla ya kutumia mbolea ili kuhakikisha wanatumia mbolea sahihi inayolingana na mahitaji ya udongo na kuongeza tija ya uzalishaji.

"Ili kupata matokeo mazuri, ni muhimu kila mkulima kupima afya ya udongo wa shamba lake badala ya kuchukua sampuli za jumla kwani itamsaidia kufanya maamuzi sahihi na kuepusha hasara," alisema Dkt Diallo.

Kauli hiyo aliitoa Mei 26,, 2025, katika mkutano na wakulima wa Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Miwa (AMCOS) cha Mkula, Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara, mkoani Morogoro, wakati wa ziara ya kikazi ya Bodi na Menejimenti ya TFRA kwa wakulima wa miwa.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza, kupokea changamoto za wakulima na kuzitafutia ufumbuzi pamoja na kuwahimiza kupima afya ya udongo ili kuongeza mavuno na kupunguza gharama zisizo za lazima.

Kwa upande wake, Meneja wa AMCOS hiyo, Clemency Mjami, aliishukuru serikali kwa kutoa ruzuku ya mbolea, akieleza jinsi ilivyosaidia kupunguza gharama kwa wakulima.

"Kupitia ruzuku hii, bei ya mbolea imepungua kutoka shilingi 120,000 hadi 68,000 kwa mfuko na kumwezesha kila mkulima kumudu gharama ya pembejeo hii muhimu" Mjami alisema.

Aliongeza kuwa, wakulima wa AMCOS hiyo wamehudumiwa kwa jumla ya mifuko 11,740 ya mbolea sawa na tani 587, zenye thamani ya ruzuku ya shilingi 182,707,521 kwa kipindi cha miaka mitatu tangu 2022/2023, mpango huo ulivyoanza kutekelezwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakulima waliielekeza shukrani zao kwa serikali na kueleza kuwa ruzuku hiyo imewasaidia katika kukuza uchumi wao na kuiomba serikali kuendelea kutoa ruzuku na kuinua ari ya kujihusisha na kilimo chenye tija miongoni mwao.

Akitoa shukrani zake, mkulima na mkazi wa kijiji cha Msofini,,Kata ya Mkula, Amanda Punguti, alisema ruzuku imewasaidia wakulima wenye hali duni kupata pembejeo na kuongeza uzalishaji.

"Ruzuku ya mbolea imekuwa mkombozi kwa wakulima wadogo. Tunaiomba serikali iendelee kutupa moyo huu wa kusaidia wakulima," alisema Punguti.

Mara baada ya kikao hicho wajumbe na menejimenti ya TFRA walitembelea kiwanda cha sukari, Kilombero kujifunza na kushauri namna bora ya kuongeza ushirikiano baina yao na wakulima wadogo wa miwa wanaowazunguka.

# HABARI KATIKA PICHA, ZIARA YA BODI NA MENEJIMENTI YA TFRA KWA WAKULIMA WA MIWA IFAKARA MKOANI MOROGORO



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Robert Mtendamema akizungumza mara baada ya kuwasili katika kiwanda cha sukari cha Kilombero mkoani Morogoro tarehe 26 Mei, 2025



Mwenyekiti wa Bodi ya TFRA, Dkt. Anthony Diallo (wa pili kutoka kushoto), wajumbe wa Bodi, Dkt Peter Shimo (kulia), Hadija Jabir (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Robert Mtendamema, (wa kwanza kulia) wakisikiliza maswali ya wakulima Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Miwa (AMCOS) cha Mkula, Mei 26,, 2025 Ifakara mkoani Morogoro













## HABARI KATIKA PICHA, ZIARA YA BODI NA MENEJIMENTI YA TFRA KWA WAKULIMA WA MIWA IFAKARA MKOANI MOROGORO









# TUNZENI HATI ZA HAKIMILIKI ARDHI, WAKULIMA SONGWE WAASWA



Wakulima na wafugaji wa kijiji cha Galula, wilayani Songwe, wametakiwa kutunza hati za hakimiliki za kimila za mashamba yao walizokabidhiwa na serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kushirikiana na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi na Halmashauri ya wilaya ya Songwe.

Akikabidhi hati hizo, Afisa Ardhi wa Wilaya hiyo, Jailo Mbembela, aliwataka wakulima kuthamini juhudi za serikali katika kuwawezesha kumiliki mashamba yao kwa mujibu wa sheria, hatua inayoongeza thamani ya ardhi na kuwapa fursa ya kupata mikopo.

Naye Meneja wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'ondya, alieleza manufaa watakayoyapata wanufaika hao kuwa ni pamoja na kupata huduma za pembejeo, mikopo kupitia kadi janja itakayounganisha taarifa zote za mkulima.

Naye Diwani wa kata ya Galula, Mikonzi Mwavilongo, alileza kuwa hatua ya kupima maeneo na kutoa hati za Hakimiliki za ardhi kumepunguza migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji wa kata hiyo na nyingine zilizofikiwa na huduma hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakulima wameishukuru serikali kwa kutimiza ahadi yake na kuzingatia makundi maalum kama wanawake, vijana, wazee na walemavu katika zoezi hilo. Jumla ya wakulima zaidi ya 3000 kutoka vijiji vinne wilayani Songwe wamekabidhiwa hati hizo.



# Habari katika picha, ugawaji wa Hati za Hakimiliki za mashamba kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe











# Wadau wa mbolea watakiwa kuzingatia huduma bora kwa wakulima

Washiriki wa mafunzo ya biashara ya mbolea wametakiwa kusikiliza na kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo ili waweze kutoa huduma bora kwa wakulima wanaowahudumia mara baada ya mafunzo hayo.

Wito huo ulitolewa na Afisa Kilimo wa Manispaa ya Morogoro, Shaban Charles, alipokuwa akifungua mafunzo ya mbolea yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Mei 12, 2025.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalifanyika katika Ukumbi wa Amabilis Center (Mgolole), mkoani Morogoro, kwa ushirikiano baina ya TFRA na wataalam kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo --- MATI Ilonga wilayani Kilosa..

Akieleza umuhimu wa mafunzo hayo, Mratibu kutoka TFRA, Azizi Mtambo, alisema, yalilenga kuwajengea uwezo wadau wa tasnia ya mbolea kuhusu matumizi sahihi, salama, na yenye tija ya mbolea, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Mamlaka wa kuimarisha huduma kwa wakulima kupitia elimu kwa wasambazaji na wauzaji wa pembejeo.

Mafunzo hayo yamehudhuriwa na washiriki 248 kutoka mkoa huo na mikoa ya Shinyanga, Dar es Salaam, Geita na Rukwa yakihusisha wafanyabiashara wa mbolea, wamiliki wa maduka ya pembejeo, wanafunzi wa vyuo, na wadau wengine ambao hawakuwahi kupata mafunzo kama hayo hapo nyuma.

Katika mafunzo hayo mada zilizowasilishwa ni pamoja na; kuwawezesha wadau kufahamu majukumu na huduma zinazotolewa na TFRA, aina za mbolea na visaidizi vyake, virutubisho vilivyopo kwenye mbolea na kazi zake na dalili za upungufu wa virutubisho katika mimea.

Mada nyingine ni pamoja na; faida ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wafanyabiashara, changamoto na makosa yanayowakumba wafanyabiashara wa mbolea, ,amna ya kupata kibali cha biashara ya mbolea kupitia Mfumo wa Kidigitali wa Fertilizer Information System (FIS) na Sheria ya Mbolea na adhabu kwa ukiukwaji wake.

Lakini pia washiriki wamefundishwa juu ya ruzuku ya mbolea na namna ya kuwa wafanyabiashara wa mbolea ya ruzuku kwa kutumia mfumo wa kidigitali wa pembejeo za kilimo na nyingine nyingi.

Mtambo alieleza kuwa kupitia mafunzo hayo, Mamlaka inalenga kuhakikisha kuwa kila mdau wa mbolea nchini anatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, huku akichangia ipasavyo katika kuongeza tija na ustawi wa sekta ya kilimo nchini.




# HABARI KATIKA PICHA, MAFUNZO KWA WAFANYABIASHARA WA MBOLEA MKOANI MOROGORO





# Imani potofu kuhusu mbolea yafutika Kishapu



Juhudi za serikali kupitia ushirikiano kati ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bodi ya Pamba na Mradi wa Building a Better Tomorrow – Youth Initiative for Agribusiness (BBT) zimesaidia kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la pamba kwa wakulima wa Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga, na kubadili mtazamo wao kuhusu matumizi ya mbolea.

Awali, wakulima wengi wa wilaya hiyo walikuwa na imani potofu kuwa mbolea inaharibu ardhi, jambo lililosababisha wao kushindwa kuzalisha kwa tija na hivyo kuchelewa kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza Mei 13,i 2025 Afisa Ugani chini ya Mradi wa BBT, Juni Ezekia Bitana, alieleza kuwa kupitia juhudi za pamoja baina ya wadau hao, wakulima walifundishwa kanuni 10 bora za Kilimo cha Pamba, ikiwa ni pamoja na elimu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Bitana alifafanua kuwa Halmashauri ya Kishapu ilipokea kifaa cha kupima afya ya udongo kilichotumika kupima mashamba ya wakulima wa mfano.

Alieleza kuwa matokeo ya vipimo hivyo yalisaidia kutoa elimu sahihi kwa wakulima kuhusu aina na kiwango cha mbolea kinachotakiwa, hatua iliyosaidia kuongeza uelewa na matumizi sahihi ya pembejeo hiyo muhimu.

"Licha ya changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, wakulima wameweza kuzalisha vizuri msimu huu na wameonyesha dhamira ya kuendeleza kilimo bora," alisema Bitana.

Wakulima wa pamba wa wilaya ya Kishapu walioshiriki katika mafunzo hayo wameeleza kuwa, awali walikuwa wakilima bila kutumia mbolea kwa hofu ya kuharibu udongo na kubaini kuwa si kweli.

Ameeleza kuwa, baada ya kupatiwa elimu, wakulima hao wameanza kutumia mbolea na kuahidi kuwa mabalozi wa kuelimisha wakulima wengine kuhusu umuhimu wa mbolea katika kuongeza uzalishaji.

Wamesema kuwa msimu huu pamba ilistawi vizuri, ambapo kila tawi lilikuwa na wastani wa vitumba 90 hali iliyowafanya kuwa na matarajio ya kuvuna maradufu ya walivyokuwa wakivuna awali, ingawa ukame uliyojitokeza mwishoni mwa msimu ulisababisha kupukutika kwa matunda na kueleza hata hivyo wanamatarajio ya kuvuna zaidi kuliko misimu ya nyuma.

# Habari katika picha wakati wa ziara ya kuwatembelea wakulima wa pamba mikoa ya Singida, Simiyu na Shinyanga





# Wazalishaji wa Mbolea waaswa kutunza na kuwasilisha Takwimu za Uzalishaji TFRA




Getrude Ng'weshemi, Kaimu Meneja wa Uhamasishaji Uzalishaji wa Mbolea na Mazingira kutoka TFRA, akifungua mafunzo ya ujazaji na uwasilishaji wa takwimu za uzalishaji wa mbolea kwa wazalishaji kutoka mikoa mbalimbali, yaliyofanyika katika Hoteli ya Tiffany Diamond, Dar es Salaam, tarehe 28 Mei 2025.

Wazalishaji wa mbolea na visaidizi vyake nchini wametakiwa kuhakikisha wanatunza na kuwasilisha takwimu sahihi za uzalishaji kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kupitia mfumo maalumu wa ukusanyaji wa data, ikiwa ni takwa la kusheria kama lilivyo kwenye Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 na Kanuni zake.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 28 Mei, 2025 na Kaimu Meneja wa Uhamasishaji Uzalishaji wa Mbolea na Mazingira wa TFRA, Getrude Ng'weshemi, wakati akifungua mafunzo ya siku moja yaliyofanyika katika Hoteli ya Tiffany Diamond jijini Dar es Salaam.

Ng'weshemi amesema, lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa namna ya kujaza na kuwasilisha takwimu za uzalishaji zitakazosaidia kuboresha ufuatiliaji na upangaji wa mipango endelevu ya sekta ya mbolea nchini.

Alisisitiza kuwa, takwimu sahihi si hitaji la kisheria pekee, bali ni nyenzo muhimu katika kufanya maamuzi yenye tija, kufuatilia maendeleo ya viwanda, kuimarisha uwajibikaji, na kupanga mipango endelevu ya uzalishaji.

Akitoa mada wakati wa mafunzo hayo, Afisa Udhibiti Ubora kutoka Kitengo cha Usajili na Leseni, Charles Alex, amewahimiza washiriki kuhakikisha wanasajili biashara zao ili kuboresha ufuatiliaji wa bidhaa zinazozalishwa na zinazotumika nchini.

Naye, Afisa Biashara wa TFRA, Godwin Tumaini aliendesha mafunzo ya vitendo kwa washiriki, akionyesha kwa undani jinsi ya kujaza fomu maalum za uwasilishaji wa takwimu za uzalishaji.

Washiriki walipongeza juhudi za TFRA katika kuwajengea uwezo na kutoa mwongozo wa kisheria na kiutendaji katika kusimamia shughuli zao za uzalishaji na kuahidi kushirikiana kwa karibu na TFRA kwa kuhakikisha taarifa sahihi za uzalishaji zinawasilishwa kwa wakati.

Akihitimisha mafunzo hayo, Ng'weshemi alitoa wito kwa washiriki kuzingatia matakwa ya kisheria ya uwasilishaji wa takwimu, akisisitiza kuwa hatua hiyo ni chachu ya maendeleo endelevu na ufanisi wa sekta ya mbolea nchini.



Afisa Biashara wa TFRA, Godwin Tumaini, akiendesha mafunzo ya vitendo kwa washiriki kuhusu ujazaji sahihi wa fomu za uwasilishaji wa takwimu za uzalishaji.

# Habari katika picha, mafunzo ya namna ya kuwasilisha takwimu za uzalishaji kwa wamiliki wa viwanda vya mbolea nchini




Washiriki wa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kukamilisha mafunzo hayo kwa mafanikio.



Washiriki wakipata mafunzo ya vitendo kuhusu mfumo wa uwasilishaji wa takwimu za uzalishaji wa mbolea, chini ya uratibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania(TFRA)

# TFRA yawafikia wakulima Mbeya DC kwa Elimu ya Matumizi Sahihi ya Mbolea

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kupitia Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya, imewapatia wakulima wa Halmashauri ya Mbeya Vijijini elimu ya matumizi sahihi ya mbolea, umuhimu wa kupima afya ya udongo, na kuhamasisha usajili wao katika mfumo wa ruzuku ya pembejeo ili kunufaika na mbolea na mbegu zinazotolewa na Serikali.



Huduma hizi zimetolewa kupitia ushiriki wa TFRA katika Maonesho ya Wakulima Festival, tukio maalum la kilimo lililoratibiwa kwa ushirikiano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Taasisi ya Dynamic Agriculture Program.

Akizungumza katika banda la TFRA, Bw. Nkundwe Mwambuga, Mwakilishi wa Ruzuku wa Mkoa wa Mbeya, amesema kuwa katika siku tatu za kwanza za maonyesho haya ya siku sita (25–30 Aprili, 2025), wakulima 11 wamehuisha taarifa zao, wakulima 30 wamesajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku ya mbolea, na zaidi ya wakulima 200 wamepatiwa huduma na elimu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Kwa upande wake, Bw. Fadhili Alisoni, Mkurugenzi Mtendaji wa Dynamic Agriculture Program, alieleza kuwa maonesho haya yameandaliwa ili kuwapa wakulima wa vijijini nafasi ya kujifunza mbinu bora za kilimo kwa kuwa wengi wao hawawezi kufika kwenye maonyesho ya kitaifa.

Alibainisha kuwa, wakulima wengi wanategemea kilimo kwa asilimia kubwa lakini wanakosa maarifa ya kitaalamu, hali inayosababisha mavuno duni licha ya juhudi zao.

Bw. Fadhili aliongeza kuwa programu hii ya elimu ya kilimo cha kisasa ni sehemu ya maono mapya ya kampuni yao, ikiwa na lengo la kufikia wilaya zote tisa za Mkoa wa Mbeya na kuchangia kuinua uchumi wa wakulima kupitia teknolojia na maarifa ya kisasa.



# TFRA yawafikia wakulima Mbeya DC kwa Elimu ya Matumizi Sahihi ya Mbolea

